**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA NNE

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE

**9 SEPTEMBA, 2016**

## MKUTANO WA NNE

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE - TAREHE 9 SEPTEMBA, 2016

### I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika alisoma Dua na kuongoza Bunge.

**MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Ramadhani Issa
2. Ndg. Neema Msangi
3. Ndg. Joshua Chamwela

### II. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:

1. OFISI YA WAZIRI MKUU:
   Swali Na. 41 : Mhe. Innocent Lugha Bashungwa
   Nyongeza: Mhe. Innocent Lugha Bashungwa.

2. OFISI YA RAIS (TAMISEMI):
   Swali Na. 42 : Mhe. Yosepher Ferdinand Komba (liliulizwa na Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda).
   Nyongeza: i) Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda
   ii) Mhe. Sixtus Raphael Mapunda
   iii) Mhe. Joseph Roman Selasini

   Swali Na. 43: Mhe. Saul Henry Amon (liliulizwa na Mhe. Fredy Atupele Mwakibete).
   Nyongeza: i) Mhe. Fredy Atupele Mwakibete
   ii) Mhe. Maftah Abdallah Nachuma
   iii) Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa

   Swali Na. 44 – Mhe. Esther Alexander Mahawe.
   Nyongeza: 1) Mhe. Esther Alexander Mahawe
   2) Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
   3) Mhe. Anthony Calist Komu

3. WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:
   Swali Na. 45 Mhe. Jamal Kassim Ali.
   Nyongeza: i) Mhe. Jamal Kassim Ali
   ii) Mhe. Salim Hussein Yusuph

Swali na. 46 : Mhe. Mwantakaje Haji Juma
Nyongeza: i) Mhe. Mwantakaje Haji Juma
ii) Mhe. Ajali Rashid Akbar

4. WIZARA YA NISHATI NA MADINI:
Swali Na. 47: Mhe. Lathifah Hassan Chande (Liliulizwa na Mhe. Cecil David Mwambe)

Nyongeza: Mhe. Cecil David Mwambe.

Swali Na. 48: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale
Nyongeza: Mhe. Vedasto Edgar Ngombale.

5. WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Swali Na. 49: Mhe. Hassan Elias Masala
Nyongeza: Mhe. Hassan Elias Masala.

Swali Na. 50: Mhe. Frank George Mwakajoka
Nyongeza: Mhe. Frank George Mwakajoka.

6. WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:
Swali Na. 51: Mhe. Najma Murtaza Giga (liliulizwa na Mhe. Khadija Hassan Aboud)

Nyongeza: Mhe. Khadija Hassan Aboud.

Swali Na. 52: Mhe. Josephine Tabitha Chagula
Nyongeza: Mhe. Josephine Tabitha Chagula.

7. WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Swali Na. 53: Mhe. Ali Seif Ungando
Nyongeza: Mhe. Ali Seif Ungando.

Swali Na. 54: Mhe. Daimu Iddi Mpakate
Nyongeza: Mhe. Daimu Iddi Mpakate.

8. WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:
Swali Na. 55: Mhe. Prof. Norman Sigalla King (liliulizwa na Mhe. Deo Kasenyenda Sanga)

Nyongeza: Mhe. Deo Kasenyenda Sanga.

## III. MATANGAZO:

Wageni mbalimbali waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na kuona namna Bunge letu linavyofanya kazi walitambulishwa.

## IV. MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na kuitaka Serikali itoe kauli kwamba Vikao vya Kamati za Bunge viendelee kukutana Dar es Salaam kwa kuwa wataalam wengi wa Serikali bado wapo Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Spika alimshauri Mbunge atumie Kanuni inayotakiwa kwa suala hilo kwani Kanuni aliyotumia haihusiani na alichokiomba.

## V. KAULI ZA MAWAZIRI:

Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dkt. Charles John Tizeba aliwasilisha Kauli ya Serikali kuhusu Hali ya Chakula Nchini.

### MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Musukuma Joseph Kasheku aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 47 na 69 akiomba Shughuli za Bunge zinazoendelea ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo muhimu la dharura kuhusu hali mbaya ya chakula na uzalishaji wa chakula nchini kufuatia kauli ya Waziri iliyotolewa Bungeni.

Naibu Spika alifafanua matakwa ya Kanuni ya 69 na kuomba kuwa Mbunge yeyote anayetaka jambo hilo lijadiliwe awasilishe Hoja mahsusi kwa ajili hiyo.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Mhe. Ummy Ali Mwalimu aliwasilisha Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016, na kutoa Hoja kuwa Muswada huo sasa usomwe kwa Mara ya Pili;

Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile, Msemaji wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016;

Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliwasilisha Maoni ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016.

### MWONGOZO WA SPIKA: (Kanuni ya 86 (6-8):

Mhe. Dkt. Abdallah Posi aliomba Mwongozo kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani anatoa maelezo ambayo yapo nje ya mjadala na hayahusiani kabisa na Muswada uliopo mezani.

Naibu Spika alielekeza Msomaji aruke sehemu husika na aende moja kwa moja kwenye Hoja. Msomaji alifuata ushauri huo na kuendelea.

Uwasilishaji wa Muswada wa Pili uliendelea kama ifuatavyo:-

- Mhe. Ummy Ally Mwalimu, aliwasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 na kisha kutoa Hoja ya kuomba Muswada huo ujadiliwe na Bunge;

- Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016;

- Mhe. Esther Nicholaus Matiko Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliwasilisha Maoni ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016.

  Wakati Msemaji wa Upinzani akiendelea, Mhe. Dkt. Abdallah Posi aliomba Mwongozo kuwa Msemaji huyo anavunja Kanuni ya 66(b)-(8) kwa kueleza Mambo yaliyo nje ya mjadala. Naibu Spika alimsihi Msemaji kuzingatia Kanuni hiyo na mjadala uliendelea.

- Naibu Spika alitumia Kanuni ya 28(2) kuongeza muda wa dakika 30 ili kumalizia hotuba ya upinzani.

## VII. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.10 mchana Naibu Spika alisitisha Kikao cha Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

## VIII. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea Saa 11.00 Jioni, mjadala wa Miswada yote miwili ulianza na wafuatao walichangia:-

1. Mhe. Susan Anselm Lyimo – CHADEMA
2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara – CHADEMA
3. Mhe. Abdallah Dadi Chikota – CCM
4. Mhe. Hamidu Hassan Bobali – CUF
5. Mhe. Dkt. Faustine Englebert Ndugulile – CCM
6. Mhe.Hussein Mohammed Bashe – CCM
7. Mhe. Boniphace Mwita Getere – CCM
8. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola – CCM
9. Mhe. Salum Mwinyi Rehani – CCM
10. Mhe. Joseph George Kakunda – CCM
11. Mhe. Anna Richard Lupembe – CCM

12. Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga – CCM
13. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola – CCM
14. Mhe. Augustino Manyanda Masele – CCM
15. Mhe. Jaku Hashim Ayoub – CCM

## IX. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 1.30 usiku Naibu Spika aliahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe 13/09/2016 Saa 3.00 Asubuhi.

**DODOMA**
**09 SEPTEMBA, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**